



Ng'ombe aliyelishwa vyema.



Maziwa zaidi



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.kari.org

Watayarishaji:

Lukuyu, B.A. Muriuki, K na Lukuyu, M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Muguga South,

S.L.P. 30148-00100

Nairobi

Simu: (066)328801/6 au 2700617

Nukulisi: (066)32348/32884

Baruapepe: narc muguga@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 22 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Ukuzaji mahindi ya chakula cha binadamu na lishe ya wanyama



Utangulizi

Utumizi wa viungo vya mahindi kulisha wanyama umekuwa kipengele muhimu kwa wakulima wadogo wanaolima na kufuga sambamba nchini Kenya. Malisho haya huchangia asilimia 24 ya jumla ya malisho ya wanyama na kufanya ukuzaji wa mahindi kwa manufaa ya mbegu na lishe ya wanyama kuwa muhimu.

Utunzaji wa mahindi kwa manufaa mawili

Ni lazima mahindi yavunwe nyakati mbalimbali ili kupata mbegu mwafaka na chakula cha wanyama cha hali ya juu. Nyakati za kuvuna ni punde mmea ufikapo urefu wa goti, wakati mahindi yana maziwa, wakati wa uloevu na wakati wa kuvuna mbegu ili kupata viungo vilivyokauka vyema.



Viungo vya mmea mahindi vilivyokauka na kuhifadhiwa

Wakulima hutumia mbinu kadhaa kupata chakula zaidi cha wanyama kama vile:

1) Kupanda mbegu nyingi

Hii inaweza kutimizwa

- Kwa Kupanda mbegu zaidi ya moja kwa kila shimo ili kupata mimea zaidi.
- Kupunguza nafasi kati ya mimea. Mbinu hizi huongezea chakula cha wanyama kwa asilimia 140.

Kupanda kwa wingi kunahitaji mikakati iwepo ya kurudisha rutuba ya mchanga.



Majani yaliyokatwa kutoka kwa mimea ya mahindi

2) Aina za mahindi zinazostahimili maradhi upotezaji wa viungo vya mahindi

Ni muhimu kutumia aina za mahindi ambazo hustahimili magonjwa vizuri ili kuhakikisha uvunaji wa viungo vya kutosha vitakavyotumiwa wakati wa kiangazi. Aina hizi za mahindi huhifadhi hadi asilimia arobaini ya viungo vya mmea mahindi (thinning na stover) ambavyo hupotea kutokana na maradhi ya virusi vya mahindi viitwavyo *Early maize streak virus disease* (MSVD)

3) Baadhi ya aina za mahindi kwa manufaa mawili yakuzwayo

Hizi ni aina ambazo:

- Zinafaa kwa mbegu na chakula cha wanyama.
- Hustahimili maradhi ya maize streak. Mfano mmoja ni KH500-43A ambayo ina majani kemkem na yenye utamu yakichemshwa.

Hukomaa baada ya muda mrefu na kwa hivyo hukua vizuri sehemu zenye unyevunyevu.



Aina ya mahindi yenye majani ya hali ya juu

Ukihimiza mbinu zilizoelzewe hapo awali, unaweza kupata maakuli yanayoweza kulisha ng'ombe wa kilo 350 kwa muda ulionyeshwa hapa:

Kiasi cha ardhi	Aina maakuli	Majani yaliyokauka (kilo)	Muda (siku)
0.17ha* Heka nukta kumi na saba	Majani yaliyong'olewa	395-759 (mia tatu tisini na tano hadi mia saba hamsini na tisa)	64-117 Siku sitini na nne hadi siku mia moja kumi na saba (miezi miwili –mitatu)
0.17ha* Heka nukta kumi na saba	Matawi ya stover	24-153 Ishirini na nne hadi mia moja hamsini na tatu	4-27 Siku nne hadi ishirini na saba (mwezi mmoja)
Wakati	Jumla		68 – 144 Siku sitini na nane hadi mia moja arobaini na nne. (miezi miwili hadi mitano)

*0.17ha ndicho kipimo wastani cha ardhi ambayo hutengewa mahindi katika sehemu za juu zenye watu wengi nchini Kenya na mazao ni ya misimu mifupi na mirefu ya mvua.